


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA  
WATOTO**



**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA - LIGULA**

**FOMU YA MKATABA WA UJENZI WA NYUMBA MBILI ZA  
WATUMISHI ZABUNI NA. ME/007/LRRH/2021-22/19 LOT 3**

**NOVEMBA, 2021**

**A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA**

1	<b>Mwajiri</b>	Abdallah M. Malela, Katibu Tawala Mkoa, S. L. P 544, Mtwara.
2	<b>Jina na anwani ya Fundi (Mwajiriwa)</b>	Rashidi Abdalla, Namba ya simu: 0683 044 733 <b>Mtwara</b>
3	<b>Eneo la Ujenzi</b>	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Ligula
4	<b>Maelezo ya Kazi kwa Ufupi</b>	Ujenzi wa Nyumba Mbili za Watumishi
5	<b>Gharama ya Ufundu</b>	Shilingi Milioni Kumi Na Tano Mia Moja na Nane Elfu Mia Nne Arobaini na Nne tu ( <b>Tsh. 15,108,444.00</b> )
6	<b>Muda wa Mkataba (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):</b>	Tarehe ya Kusaini: 22/11/2021. Muda: Siku 120 (miezi Minne) 1. Tarehe ya Kuanza Kazi: Muda wowote baada ya kusaini Mkataba. 2. Tarehe ya Kumaliza Kazi 30/04/2022.
7	<b>Masharti ya malipo:</b>	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Fundi atalipwa <b>10%</b> ya gharama za ufundu kama malipo ya awali (Advance Payment)</li> <li>• Fundi atalipwa kwa awamu <b>Nne</b> kwa kila kazi zitakazokuwa zimekamilika na kukaguliwa.</li> </ul>

**B: MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA**

1. Mwajiri anakusudia kumwajiri "Mjenzi" **KUJENGA NYUMBA MBILI ZA WATUMISHI.**
2. Mjenzi amekubali kujenga "**NYUMBA MBILI ZA WATUMISHI** kwa gharama ya **Shilingi Milioni Kumi Na Tano Mia Moja na Nane Elfu Mia Nne Arobaini na Nne tu (Tsh. 15,108,444.00) pamoja na Kodi**

3. Mwajiri atatoa vifaa (Building Materials) vitakavyohitajika kwa ajili ya ujenzi kwa kuzingatia maelekezo ya Msimamizi wa Mradi (Project Manager);
4. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na Mwongozo wa Msimamizi Mkuu (Project Manager) kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi;
5. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kumtaka kulipa hasara zote zilizotokana na uzembe au makusudi;
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na wanakuwa na uaminifu wa hali ya juu. Aidha, ajira za watoto haziruhusiwi kabisa;
7. Fundi atawajibika kwa tabia zote zisizokubalika kama vile wizi, uharibifu wa mali eneo la ujenzi na vitendo vyote vitakavyofanywa na mafundi wake na mtu ye yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake. Aidha, atawajibika kwa kutoa fidia kwa watumishi wake ikiwa watapata ajali kazini;
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa **safi** na salama na pia atakapomaliza kazi, ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama;
9. Kiasi cha asilimia tano (5%) ya kiasi cha Mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa mwezi mmoja baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho wa pamoja kufanyika na pale itakapoonekena kuna marekebisho yatafanywa kwa gharama za fundi;
10. Fundi anatakiwa kuwepo eneo la ujenzi muda wote wa utekelezaji wa mradi;
11. Fundi anatakiwa kuandaa mpango kazi na kuuwasilisha kwa mwajiri wakati wa utekelezaji wa mradi na anatakiwa kuufuata ipasavyo;

**12. Ucheleweshaji wa Kazi:**

- **Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi**, fundi atalipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo;
- **Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri (kutokana na fedha au vifaa)**, Fundi ataongezewa muda sawa na kipindi chote kazi iliposimama;

**13. Uvunjwaji wa Mkataba:**

Mkataba utavunjwa iwapo;

- Fundi au mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihuisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya eneo la ujenzi.;
- Fundi au fundi msaidizi hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya *Project Manager* ambaye ni Mhandisi wa Mkoa;
- Fundi akichelewesha kazi kwa muda wa mwezi 1 bila sababu yoyote ya msingi.

**MWAJIRI:**

Jina ... *ABDAAUH M. MAECLA*

Saini..... *Shahid*

Cheo: *RAS*

Tarehe... *22/11/2021*  
KATIBU TAWALA MKOA  
MTWARA

**FUNDI:**

Jina *RASHIDI A. RAJABU*

Saini *Ras*

Cheo: *FUNDI*

Tarehe *17/11/2021*

**SHAHIDI WA MWAJIRI**

Jina *ABUBAKARI S. MSANGI*

Saini *Shahid*

Cheo: *AFISA SHERIA MKUYI*

Tarehe... *22/11/2021*

**SHAHIDI WA FUNDI**

Jina ... *MAHAMUDU LIWALI*

Saini *Mahamud*

Cheo: *MFANTYA BIASHARA*

Tarehe *17/11/2021*

